



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**



**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA**

tafadhali taja:

Kumb.Na .HW/MPW/S10/51 VOL II/67

19/04/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

1.0 UTANGULIZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa baada ya kupokea kibali cha ajira mbadala chenye Kumb Na. **FA.170/360/01/"A"/29** cha tarehe 15/03/2022 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora anawatangazia Wananchi wote Raia wa Tanzania wenye sifa zinazohitajika kuomba kujaza nafasi wazi kama zifuatazo:-

1.1 MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (NAFASI 4)

1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne na kuendelea.
- Awe amefuzu mafunzo ya Astashahada/Cheti NTA/LEVEL 5 katika moja ya fani zifuatazo: Utawala Sheria, Sayansi ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii, kutoka Chuo cha Usimamizi wa Serikali Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali .

1.3 KAZI NA MAJUKUMU

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji .
- Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao kuwa mlinzi wa Amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
- Kuratibu na kusimamia upangaji na utelekezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kijiji
- Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi katika kuandaa na kutekeleza mkakati wa kuondoa njaa umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaaluma katika Kijiji
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji
- Mwenyekiti wa kikao cha wataalam waliopo katika Kijiji
- Kupokea kusikiliza na kutatua malalamiko ya migogoro ya Wananchi
- Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji na
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata

S.L.P 12 Mpwapwa, Simu +255026-2321122, Nukushi, +255-026-2320122, Barua

Pepe, info@mpwapwadc.go.tz, ded@mpwapwadc.go.tz, Tovuti, www.mpwapwadc.go.tz

